

MANABII!!

Katika bustani na majumba ya kukodi  
Katika mijengo kutokana na udokozi  
Matapeli wadondokwao na ulibwende  
Wanabubujikwa na ma-povu vinywani  
Sauti za jadhba za “Semeni Haleluya!”  
Zinapanda angani kama makombora  
Waumini waliofungwa fahamu pingu  
Wanaporwa kimachomacho ja mazuzu  
Wanakengeushwa “kupanda mbegu”  
Masikioni, wamejazwa gube tamutamu:  
Wanaonyongwa na ukosefu wa ajira  
Watapata kazi za malipo maangavu,  
Waendeshao Volkswagen Beetle  
Watamiliki LandCruiser VX mpya,  
Wenye ulemavu sugu tangu utotoni  
Ulemewa utapuliziwa mbali na upepo,  
Waliotafuta wachumba bila kufua dafu  
Watapata waandani wa kumezewa mate,  
Wenye miji-ya-uzazi iliyokithiri utundu  
Upesi watajifungua mapachamapacha,  
Wanaougua maradhi yanayobeza tiba  
Watapona pasi kuongea na daktari,  
Hata kurejesha duniani waliozimika uhai  
Hilo, abadani, usidhani ni suala muhali  
Bora zitumike ndimi, kwa sauti mtitimo!

Wajitwazao kuwa watumishi wa Mungu  
Wakiwemo walioingia shule za shinani  
Lo! Kichungi cha mitihani kikawachuja

Wakaishia kuwa masimbi katika jamii,  
Zumbukuku bila mafundisho ya kidini  
Mabazazi wasioelewa kamwe Bibilia,  
Leo, kwa unyanyanyi usiotumia mababu  
Kwa wizi mbele ya macho wazi ya sheria  
Ndio waendeshao masigingi meusi mapya  
Wakisindikizwa na askari wenye AK 47  
Barabarani wakitisha madereva kwa inda,  
Ndio waishio mitaa ya kijani kibichi kizito  
Nyumba zao zikifurika bidhaa za anasa,  
Ndio watembeao kwa mikiki na mikogo  
Wakiandamwa na walinzi tumbitumbi,  
Ndio wajichaguliao vyeo vinavyometa:  
Mara ni wachungaji wagavi wa ulokole  
Au ni maaskofu tarishi halisi wa mbingu,  
Wengine, bila kujali mjeledi wa Mungu  
Daima wakinywa damu ya watesekao  
Wanajiita manabii wakuu kuliko wote!

#### **Kithaka wa Mberia**

---

Kwa mengi kuhusu mwandishi, ikiwa ni pamoja na maandishi yake, tembelea:

**[www.marimbapublications.co.ke](http://www.marimbapublications.co.ke)**